HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA
KUMBUKUMBU ZA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ROBO YA KWANZA (JULAI - SEPTEMBA, 2023) ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA LEWIS KALINJUNA
TAREHE 30-31. 10.2023

A. WAJUMBE

WALIOHUDHURIA:

1.	Mhe. Elias R. Masumbuko	Mstahiki Meya (Mwenyekiti)
2.	Mwl Alexius R. Kagunze	Mkurugenzi wa Manispaa (Katibu)
3.	Mhe. Zamda S. Mwebea	Naibu Meya
4.	Mhe. Reuben M. Dotto	Mjumbe
5.	Mhe. Hassan R. Mwendapole	Mjumbe
6.	Mhe. Reuben N. Kitinya	Mjumbe
7.	Mhe. Mussa E. Andrea	Mjumbe
8.	Mhe. John P. Kisandu	Mjumbe
9.	Mhe. Enock C. Lyeta	Mjumbe
10.	Mhe. Moshi H. Kanji	Mjumbe
11.	Mhe. James M. Matinde	Mjumbe
12.	Mhe. Sheilla D. Mshandete	Mjumbe
13.	Mhe. Paschazia C. Seni	Mjumbe
14.	Mhe. Zuhura Waziri	Mjumbe
15.	Mhe. Gulamhafeez Mukadam	Mjumbe
16.	Mhe. Picca N. Chogero	Mjumbe
17.	Mhe. Peter J. Kwoliba	Mjumbe
18.	Mhe. Mariam L. Nyangaka	Mjumbe
19.	Mhe. Victor Y. Mkwizu	Mjumbe
20.	Mhe. Msabila M. Kulwa	Mjumbe
21.	Mhe. Esther F. Makune	Mjumbe
22.	Mhe. Ezekiel J Sabo	Mjumbe
23.	Mhe. Juma M. Nkwabi	Mjumbe
24.	Mhe. Victor T. Mmanywa	Mjumbe

B. WASIOHUDHURIA

1.	Mhe. Patrobas Katambi (MB)	Kwa taarifa
2.	Mhe. Lucy Mayenga (Mbunge VM)	Kwa taarifa

C. WATAALAM

1. Getruda Gisema	Mkuu wa Divisheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu.
2. Lenard Chepe	Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA.
3. Emmanuel Kabelwa	Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe.
4. Joseph Kafumu	Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Utamaduni, Michezo na Vijana.
5. Jesca Kipingu	Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.
6. Mensaria Mrema	Mkuu wa Divisheni ya Mipango na uratibu.
7. Peter Chuwa	Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani.
8. Octavina Kiwone	Mratibu TASAF
9. Ezra Manjerenga	Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhifadhi wa Maliasili na Mazingira.
10. Richard Massawe	Mthibiti Ubora.
11. Salu Ndongo	Afisa Mfawidhi wa Ofisi ya Ardhi Manispaa.
12. Mary S. Maka	Mkuu wa Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi
13. Lucy Sewe	Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi
14. Naely Elias	Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji
15. Charles Kafutila	Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Elimu Sekondari.
16. Kishenyi Mulokozi	Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu
17. Revocatus Lutunda	Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi
18. John Tesha	Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii.
19. Kuchibanda K. Snatus	Mkuu wa Kitengo cha usimamizi wa Taka na Usafi wa Mazingira.
20. Dorice Dario	Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria.
21. Eng Kassim Thadeo	Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Miundombinu, maendeleo ya Vijiji na Miji.
22. CPA Sunday Nkwambi	Mhasibu wa Mapato

D. WAALIKWA

1. Eng CPA Andrew Kifua	-	Kny RAS
2. Neema Rwegashora	-	Kny DAS
3. Ibrahim M. Makana	-	AAS-MMI
4. ASP Hussein Balige	-	Kny OCD
5. LT Col Ford J.Mwakasege	-	MJA
6. SSP Theophil Ngimbwa	-	DPO
7. INSP Elizabeth Kaka	-	DIO
8. Santus J. Mang'ee	-	DBC
9. Capt HK Kova	-	A/Base
10. Salma Machibya	-	Kny DSO

11. S/SGT Masoud M. Mwagilo - Kny DFO
12. Anold Makombe - M/Kiti CCM (W)
13. Ally Shabani - Katibu CCM (W)
14. Samwel Jackson - Katibu wa Mbunge

E. WAKUU WA TAASISI

1. Nkinda Senni - RUWASA
2. Eng Daniel Ojwando - TEMESA
3. Eng Yohana William - TARURA
4. Eng Wilfred Julius - SHUWASA

F. WATENDAJI WA KATA

1. Joshua Masengwa - Mtendaji wa Kata ya Ndala
2. Costantine M. Masalu - Kaimu Mtendaji wa Kata ya Masekelo
3. Gabriel Walinguzo - Mtendaji wa Kata ya Mwawaza
4. Mayala Ibrahim - Mtendaji wa Kata ya Kitangili
5. Bundala Shija - Mtendaji wa Kata ya Chamaguha
6. Patrick M. Dotto - Mtendaji wa Kata ya Ibinzamata
7. Mathias Masalu - Mtendaji wa Kata ya Mjini
8. Christina Maige - Kaimu Mtendaji wa Kata ya Kambarage
9. Gaudiozi K. Mwombeki - Mtendaji wa Kata ya Ngokolo
10. Ponsian Ngodita - Mtendaji wa Kata ya Chibe
11. Irene D. Mshandete - Mtendaji wa Kata ya Ibadakuli
12. Adella Mukinga - Mtendaji wa Kata ya Kizumbi
13. Mahiba Pastory - Mtendaji wa Kata ya Lubaga
14. Michael Joshua - Mtendaji wa Kata ya Mwamalili
15. Timothy A. Timoth - Mtendaji wa Kata ya Kolandoto
16. Mwakaluba Jacob - Mtendaji wa Kata ya Old Shinyanga

F: AFISA TARAFA

1. Neema Mukandala - Afisa Tarafa ya Old Shinyanga
2. Gregory Kachira - Afisa Tarafa ya Ibadakuli
3. Simon Mashishanga - Kaimu Afisa Tarafa ya Mjini

G : WAANDISHI WA HABARI.

1. Marco Maduhu - NIPASHE
2. Hyasinta Ludovick - Faraja FM
3. Moshi A. Ndugulile - Clouds TV & FM
4. Jerry Michael - DELLAH TV
5. Michael Abel - WASAFI FM
6. Arnold Rukiza - SHY-MC

SEKRETARIETI

1. Macelina Bwathondi	Mwandishi wa Vikao
2. Esther Daudi	Mwandishi wa Vikao
3. Georgia Kayenze	Katibu Mahsusi

Agenda za kikao zitakuwa kama ifuatavyo:-

Siku ya kwanza tarehe 30.10.2023

1. Maswali ya papo kwa papo.
2. Kufungua mkutano
3. Kuthibitisha agenda za mkutano.
4. Kupokea na kujadili taarifa za kwenye Kata kutoka kwa Madiwani wa Kata husika Pamoja na majibu ya changamoto za Kata kwa kipindi cha Nne.
5. Kuahirisha kikao

Siku ya pili tarehe 31.10.2023

6. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa Mkutano wa Baraza la Madiwani wa kawaida wa tarehe 09-10.08.2023.
7. Kupokea Mihtasari ya Kamati za Kudumu kwa robo ya Nne ya mwaka 2022/2023
   - Kamati ya Kudhibiti UKIMWI tarehe 14.07.2023
   - Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu 19.07.2023.
   - Kamati ya Mipango Miji na Mazingira 20.07.2023.
   - Kamati ya Fedha na Utawala 22.07.2023, 24.08.2023, na 15.09.2023.

8. Kupokea taarifa za utekelezaji wa Idara mbalimbali za kamati za kudumu kwa robo ya nne 2023/2024.
   - Kamati ya kudhibiti UKIMWI
   - Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu
   - Kamati ya Mipango miji na Mazingira
   - Kamati ya Fedha na Utawala

9. Taarifa kutoka kwa Mkurugenzi kama zipo.
10. Kufunga kikao.

AGD Na.01:2023/24 **MASWALI YA PAPO KWA PAPO**

Kumb: BAR.01.1.1 Katika Mkutano wa Baraza la Madiwani wa kupitia taarifa ya robo ya kwanza 2023/2024 Mwenyekiti aliwakaribisha Wajumbe kuuliza maswali ya papo kwa papo kama ifuatavyo;

Kumb: BAR.01.1.2 **Swali:** Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ina mkakati gani wa kujenga Shule ya Sekondari Galamba ili kupunguza changamoto ya Wanafunzi kutembea umbali mrefu wa zaidi ya Kilometa 10 kutoka Shule ya Sekondari Kolandoto **.**

Jibu: Ufafanuzi ulitolewa kuwa Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia wataalam wake wa Idara ya Elimu walipewa jukumu la kupita na kukagua ili kubaini maeneo yenye uhitaji mkubwa wa kuanzishwa Shule mpya za Sekondari na Msingi.

Kumb: BAR.01.1.3 **Swali:** Ni lini Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga itakamilisha miradi ya kimkakati**.**

Jibu: Ufafanuzi ulitolewa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga tayari ilishaandaa orodha ya vipaumbele kwa miradi yote ambayo haijakamilika. Kwa kuanza itaanza na miradi mkakati ambayo haijakamilika kama Soko Kuu na Soko la Ibinzamata

Kumb: BAR.01.1.4 **Swali:** Ni lini Ofisi ya Mkurugenzi itawezesha uendeshaji wa Ofisi za Kata

Jibu: Ufafanuzi ulitolewa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kwenye mpango na Bajeti ya 2023/2024 ilitenga fedha ya kuwezesha uendeshaji wa Ofisi za Kata. Aidha Halmashauri itaendelea kupeleka fedha kadri zinavyopatikana.

AGD Na.02:2023/24 **KUFUNGUA MKUTANO**

Kumb: BAR.01.2 Mwenyekiti alifungua Mkutano wa Baraza la Madiwani robo ya Kwanza saa 05.20 asubuhi kwa kuwakaribisha Wajumbe, Kamati ya ulinzi, Waandishi wa Habari na Wananchi katika Mkutano wa Baraza la Madiwani.

AGD Na.03: 2023/24 **KUTHIBITISHA AGENDA ZA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 30-31.10.2023.**

Kumb: BAR .01.3 Jumla ya agenda 10 zilithibitishwa kwenye Mkutano wa kawaida wa wa Baraza la Madiwani.

AGD Na.04 :2023/24: **KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA ZA KWENYE KATA KUTOKA KWA MADIWANI WA KATA HUSIKA.**

Kumb: BAR.01.4.1 Wajumbe waliwasilisha taarifa na changamoto za kila Kata husika na walionesha utatuzi wa Changamoto hizo, Wajumbe walielekeza kuwa timu ya Menejimenti kwa kushirikiana na Waheshimiwa Madiwani kushirikiana katika kutatua changamoto hizo.

Kumb: BAR.01.4.2 Aidha Wajumbe walihitimisha taarifa za utekelezaji wa Kata kwa kuweka msisitizo katika mambo yafuatayo;

- Ufuatiliaji uendelee kufanyika kwa Wateja wa CHF iliyoboreshwa ili kubaini tatizo linalopelekea wateja hao kutokuonekana kwenye mfumo.
- Kuweka mfumo mzuri wa matangazo yanayohusu taarifa ambazo Wananchi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga wanapaswa kuzijua.
- Matangazo ya zabuni yawekwe katika Ofisi zote za Kata ili Wananchi wote wapate uelewa wa zabuni zinazotangazwa.
- Suala la ulinzi wa Shule Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga itunge sheria ndogo ndogo itakayowabana Wazazi kuchagia fedha za ulinzi katika Shule za Msingi na Sekondari.
- Kata ambayo inahitaji kuanzisha mradi wa Shule waanze kwa kuchangia kama Kata kwa kukusanya nguvu za Wananchi.

AGD Na.05 :2023/24: **KUAHIRISHA KIKAO**

Kikao cha kujadili taarifa za Kata kiliahirishwa saa 7:20 mchana

SIKU 2 **31.10.2023**

AGD Na.06:2023/24: **KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 09-10.08.2023.**

Kumb:BAR.01.6 Muhtasari wa Mkutano wa Baraza la Madiwani wa tarehe 09-10.08.2023. ulisomwa ukurasa kwa ukurasa na wajumbe kuridhia kuwa yaliyomo ndiyo yaliyojadiliwa na hivyo ulithibitishwa na kuwa kumbukumbu halali ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kwa Mwenyekiti na Katibu kusaini Muhtasari huo.

AGD Na.07:2023/24: **KUPOKEA MIHTASARI YA KAMATI ZA KUDUMU YA ROBO YA NNE 2022/2023.**

Kumb:BAR.01.7.1 Kupokea Mihtasari ya Kamati za Kudumu kwa robo ya Nne ya mwaka 2022/2023 ambayo tayari ilishathibitishwa katika vikao vya Kamati vilivyofanyika;

- Kamati ya Kudhibiti UKIMWI tarehe 14.07.2023
- Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu 19.07.2023.
- Kamati ya Mipango Miji na Mazingira 20.07.2023.
- Kamati ya Fedha na Utawala 22.07.2023, 24.08.2023, na 15.09.2023

Kumb:BAR.01.7. 2 Wajumbe waliipokea Mihtasari ya Kamati za kudumu na kuridhia kuwa kumbukumbu halali ya vikao vya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga.

AGD Na.08:2023/24: **KUPOKEA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA IDARA MBALIMBALI ZA KAMATI ZA KUDUMU KWA ROBO YA KWANZA 2023/2024**.

Kumb:BAR.01.8.1 Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Divisheni na Vitengo mbalimbali vilivyo chini ya Kamati za Kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ambazo ni Kamati ya Uchumi Afya na Elimu, Kamati ya Mipango Miji na Mazingira, Kamati ya Kudhibiti UKIMWI, Kamati ya Fedha na Utawala kwa robo ya kwanza 2023/2024 iliwasilishwa kwa Wajumbe. Wajumbe waliipokea taarifa na kuijadili.

Kumb:BAR.01.8.2 **Wajumbe walihoji kuhusu Wakandarasi wanaofanya kazi katika miradi ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kama wanatenga bajeti kwa ajili ya kuelimisha kuhusiana na maambukizi ya UKIMWI.**

Ufafanuzi ulitolewa kuwa Elimu ya HIV/ UKIMWI hutolewa katika miradi yote hasa hasa miradi ya utengenezaji wa madaraja. Ufuatiliaji ulifanyika katika maeneo yote wanayofanya kazi wakandarasi ili kuhakikisha wanatoa Elimu.

Kumb:BAR.01.8.3 **Ni lini Wananchi waliopimiwa Ardhi katika maeneo ya Ndala, Kizumbi na Ibadakuli watapewa namba zao za upimaji.**

Ufafanuzi ulitolewa kuwa upimaji wa urasimishaji ulikuwa ukifanyika katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga (Ndala- Mlepa, Kizumbi- Iwelyimo na Ibadakuli – Mpera A). Wananchi wote ambao wamerasimishiwa makazi yao katika maeno tajwa watakuwa wamepewa namba za upimaji kufikia robo ya tatu 2023/2024.

Kumb:BAR.01.8.4.1 **Hoja kuhusu Wafanyabiashara kwenda kufanya biashara katika Masoko waliyopangiwa.**

Wajumbe walieleza kuwa uwekwe mkazo wa Wafanyabiashara wote kwenda kufanya biashara katika maeneo yao waliyopangiwa. Kwa Soko la Mitumbani na Soko la nguzo nane, Wafanyabiashara wote waingie ndani wasifanyie biashara nje ya soko pia Kwa Wafanyabiashara wa mbao waelekezwe kwenda kwenye maeneo ambayo wanatakiwa kuuza mbao hizo.

Kumb:BAR.01.8.4.2 Baada ya majadiiano ya kina Wajumbe walielekeza kuwa Halmashauri kuhakikisha**,** Wafanyabishara wote waelekezwe kwenda kwenye masoko waliyopangiwa, kwa soko la mitumbani na Nguzo nane wafanyabiashara wote wasifanyie biashara nje ya soko.

AGD Na.09:2023/24: **TAARIFA KUTOKA KWA MKURUGENZI.**

Kumb:BAR.01.9.1.1 **TARURA**

Taarifa iliwasilishwa kuwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini (TARURA) Manispaa ya Shinyanga ina Mtandao wa Barabara wenye urefu wa Km 780.184, kilometa 201.444 ni Barabara zinazounganisha Kata na zinazounganisha Tarafa na Wilaya jirani (collector Roads) Kilometa 578.74 ni Barabara zinazounganisha Kata na Vijiji (feeder Roads). Aidha Halmashauri ina mtandao wa km 22.707 za lami, kilometa 184.714 za changarawe na kilometa 574.763 za udongo.

Kumb:BAR.01.9.1.2 Kwa Mwaka wa fedha 2023/2024 TARURA Manispaa ya Shinyanga ilitengewa TSh 2,932,810,000.00 katika fedha hizi, fedha za matengenezo ya Barabara ni Sh 1,432,810,000.00 fedha za jimbo ni Sh 500,000,000.00 na fedha za tozo ya mafuta ni Sh 1,000,000,000.00

Aidha fedha zilizopokelewa ni jumla ya TSh 72,566,900.00 sawa na asilimia 2.5%.

Kumb:BAR.01.9.1.3 **Ni lini Barabara ya kutoka Ndala kwenda Hospital ya Rufaa ya Shinyanga itatengenezwa kwa kiwango cha lami.**

Barabara ya kuelekea Hospital ya Rufaa haijawekwa kwenye Bajeti. Kwa wakati huu TARURA itaendelea na matengenezo madogo madogo.

Kumb:BAR.01.9.1.4 **Wajumbe walihoji kuhusu Barabara na Daraja la Kitangili ni lini ukamilishaji wake utafanyika.**

Ufafanuzi ulitolewa kuwa kazi zilizosalia kukamilika kwenye madaraja ya Kitangili. Kazi hizo zitakamilika tayari zipo kwenye mpango na bajeti 2023/2024 na kazi hizo zipo hatua ya manunuzi.

Kumb:BAR.01.9.1.5 **Wajumbe walihoji kuhusu matengenezo ya barabara ya Usongo na Igalukilo kufuatia mvua kubwa zinazoendelea.**

Ufafanuzi ulitolewa kuwa eneo la Busongo na Igalukilo tayari lilishawasilishwa Makao Makuu kama maeneo hatarishi wakati wa mvua za Elnino.

Kumb:BAR.01.9.2.1 **RUWASA**

Taarifa iliwasilishwa kuwa kipindi cha utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa fedha 2023/2024 kwa kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Septemba, 2023 RUWASA iliendelea kushirikiana na Mkandarasi anayejenga mradi wa SGR ikiwa ni Pamoja na kusimamia kazi ambayo ilijitokeza ya kuhamisha njia ya Bomba eneo ambalo ilipita reli ya SGR hususani eneo panapojengwa Daraja la reli ambapo kazi hii ilipangwa kukamilika tarehe 15 Novemba, 2023 na gharama zake zinagharamiwa na Mkandarasi wa SGR.

Kumb:BAR.01.9.2.2 Wajumbe walipokea taarifa na kueleza kuwa RUWASA wafike katika eneo linalojengwa magati katika Kata ya Chibe ili kurekebisha magati yanayovuja/kumwaga maji.

Kumb:BAR.01.9.3.1 **SHUWASA**

Taarifa iliwasilishwa kuwa Mamlaka ya Majisafi na usafi wa Mazingira Shinyanga inatekeleza miradi 2 ndani ya eneo la Manispaa ya Shinyanga hadi kufikia mwishoni mwa robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/2024. Fedha za utekelezaji wa miradi hii zilitolewa na Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Maji.

Kumb:BAR.01.9.3.2 Kiasi cha TSh 113,840,500.00 kilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa mtandao wa maji safi kwa eneo la Mwanubi Kata ya Kolandoto. SHUWASA ilipokea na kulipa kiasi cha shilingi 32,521,932.00 ikiwa ni sawa na asilimia 28 ya gharama za ujenzi wa mradi. kiasi kinachodaiwa Sh 79.688,350.00 ujenzi umekamilika kwa asilimia 100 na mradi unatoa huduma.

Kumb:BAR.01.9.3.3 Kiasi cha Sh 279,465,134.40 kilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa majisafi eneo la Bugayambelele Kata ya Kizumbi. SHUWASA ilipokea na kulipa kiasi cha shilingi 212,474,474.54 ikiwa ni sawa na asilimia 76 ya gharama za ujenzi wa mradi. Kiasi kinachodaiwa 81,248,647.46 ujenzi umekamilika kwa asilimia 100 na mradi unatoa huduma.

Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa.

Kumb:BAR.01.9.3.4 **Wajumbe walihoji ni sababu gani inayopelekea magati ya maji yanafungwa wakati kuna mikataba iliyowekwa baina ya SHUWASA na RUWASA.**

Ufafanuzi ulitolewa kuwa Magati yanafungwa kwa sababu Wananchi waliofunga mkataba hawalipi fedha kama walivyokubaliana kwenye mkataba na hivyo kutengeneza madeni makubwa.

AGD Na.10:2023/24: **KUFUNGA MKUTANO**

Kumb:BAR.01.10 Mwenyekiti alifunga Mkutano saa 8:30 mchana kwa kuwashukuru Wajumbe, waalikwa, Waandishi wa Habari, Wananchi pamoja na Wataalam kwa kushiriki vizuri Mkutano wa Baraza la Madiwani.

KUMBUKUMBU HIZI ZIMETHIBITISHWA NA

_____ _____

Mwl Alexius R. Kagunze Mhe. Elias R. Masumbuko

KATIBU **MWENYEKITI**

TAREHE_____